# MTIHANI WA PAMOJA WA MOKASA

**2021**

**KIDATO CHA NNE**

**102/3 - KISWAHILI - Karatasi ya 3**

**FASIHI**

**JUNI - JULAI 2021 - Muda: Saa 2 ½**

---

Jina ………………………………………………. Nambari ya Mtahiniwa ……………………

Sahihi ……………………………. Tarehe …………………………………….....

---

Maagizo

*(a)* *Andika jina lako na nambari yako ya mtihani katika nafasi ulizoachiwa hapo juu.*
*(b)* *Tia sahihi yako kisha uandike tarehe ya mtihani katika nafasi ulizoachiwa hapo juu.*
*(c)* *Jibu maswali manne pekee.*
*(d)* *Swali la **kwanza** ni la lazima.*
*(e)* *Maswali hayo mengine yachaguliwe kutoka sehemu nne zilizobaki: yaani; Riwaya, Ushairi na Fasihi simulizi*
*(f)* *Majibu yote lazima yaandikwe kwa lugha ya Kiswahili.*
*(g)* *Majibu yote sharti yaandikwe kwenye nafasi ulizoachiwa katika kijitabu hiki cha maswali.*
*(h)* *Karatasi hii ina kurasa 5 zilizopigwa chapa.*
*(i)* *Watahiniwa ni lazima wahakikishe kwamba kurasa zote za karatasi hii zimepigwa chapa sawasawa na kuwa maswali yote yamo.*

---

**Kwa matumizi ya mtahini pekee**

| Swali | Upeo | Alama |
|---|---|---|
| 1 | 20 | |
| 2 | 20 | |
| 3 | 20 | |
| 4 | 20 | |
| 5 | 20 | |
| 6 | 20 | |
| 7 | 20 | |
| Jumla | 80 | |

for free exams visit www.freekcsepastpapers.com

## SEHEMU A: RIWAYA

**Asumpta Matei:** *Chozi la Heri*

1. Lazima

Kipi kinachowavuta raia kuhamia ughaibuni? Angeuliza nafsi yake pale ambapo mzigo wa simanzi na ukiwa ulipokilemea kifua chake. Je, ni huo mshahara mnono unaowageuza kuwa watumwa wa kufanya kazi kidindia ati kwa kudai kuwa nchi za ughaibuni ni *twenty-four-hour economies?*

a. Eleza muktadha wa dondoo hili (Alama 4)
b. Huku ukitolea mifano maridhawa, fafanua mbinu nne za kimtindo zinazojitikeza katika dondoo hili (Alama 4)
c. Eleza changamoto inayomkumba msemaji katika dondoo hili(Alama 2)
d. Fafanua jinsi maudhui yanayojitokeza katika dondoo hili yameshughulikiwa kwingineko riwayani. (Alama 4)
e. Fafanua umuhimu wa mandhari katika kuijenga riwaya hii kwa kurejelea Msitu wa Mamba (Alama 8)

for free exams visit www.freekcsepastpapers.com

## SEHEMU B : TAMTHILIA

***Pauline Kea*** **: Kigogo**

**Jibu swali la 2 au la 3**

2. Ama ale hizo falsafa zake! Udongo haubishani na mfinyanzi.
a. Eleza muktadha wa dondoo hili (Alama 4)
b. Tambua na ueleze tamathali mbili za usemi katika dondoo hili (Alama 4)
c. Eleza umuhimu wa msemaji katika kuijenga tamthilia hii kwa hoja zozote nne (Alama 4)
d. Eleza maudhui manne yanayojitokeza katika dondoo hili (Alama 8)

3. a)Jimbo la Sagamoyo limetawaliwa na uozo mwingi. Tetea kauli hii. (Alama 10)
b) Eleza mbinu zifuatazo za kimtindo jinsi zilivyotumika katika tamthilia ya Kigogo :
i) Kinaya (Alama 5)
ii) Jazanda (Alama 5)

## SEHEMU C : USHAIRI

**Jibu swali la 4 au la 5**

4. Soma shairi linalofuata kisha ujibu maswali:

Nakumbuka kwa dhiki Mto Monyara
Tuliochelea kukaribia kingo zake
Tukatulia kwanza; ukakamavu kujihamia
Kwa kunyenyekea wingi wa yake maji
Yaliyojiendea utadhani yamesimama.

Ni katika mto huu
Ambapo samaki wakubwa tulivua
Maguo kuyatakasa japo kwa kuunyemelea
Na walevi stadi wakachelea kuuvuka
Ulipofura na kupita kwa kiburi
Kwa kushiba maji yake
Yaliyofanya mawimbi madogo.

Ni hapa ambapo marehemu nyanya
Mkono alinishika na njia kuniongoza
Juu la ulalo wa miti
Vikapu vyetu hewani vikielea;
Mimi nikishika change kwa mkono mmoja
Naye akikiachilia chake kujishikisha kichwani
Masafa baina yetu na mtambo
Uliokwenda kwa nguvu za maji
Tuliyapunguza kwa kila hatua tulopiga.

Ni katika mto huu ambapo
Samaki tuliowavua tuliwapasua na kuwasafisha
Na hivyo kuuficha umaskini wetu
Ulotuzuia kununua mnofu wa bucha
Ni hapa ambapo wanawake walifika
Mawe ya kusagia kupata
Ni katika mtu huu ambapo
Waumini walifika kutakaswa kwa ubatizo
Baada ya ulevi, usinzi na kufuru nyinginezo.

Ni hapa ambapo ilisimuliwa kuwa
Hata wachawi walifika kufanya vitimbi vyao
Baada ya utawala wa jua kumezwa na nguvu za giza
Sasa Monyara niloijua haipo tena
Zimebaki kingo zilizokaukiana
Kama uso wa mrembo aliyekosa mafuta
Siku ayami.

Mti huu ambapo pembeni mwake
Watoto walipashwa tohara
Maji yake yakishangia, umekonda
Na mbavu zake nje kutoa
Na sasa vitoto vikembe vinazikanyaga
Vikijiendea zao kusaga mahindi
Juu mlimani
Katika mtambo wa Kizungu
Usioisha kulalamika
Nao wanawake hawaji tena

for free exams visit www.freekcsepastpapers.com

Kutafuta mawe ya kusagia wimbi
Imebaki njia ya walevi warejeao nyumbani
Nayo miti iliyosimama wima ukingoni
Iliisha kuanguka kwa kuleweshwa na pumzi za walevi
Wasioisha kupita hapa.

**Maswali:**

a. (i) Hili ni shairi la aina gani? (alama 1)
   (ii) Thibitisha jibu lako katika (i) (alama 2)
b. Bainisha tamathali tatu za usemi zilizotumiwa katika shairi hili. (alama 3)
c. Linganisha sifa za zamani na za sasa za Mto Monyara. (alama 3)
d. Andika mifano miwili ya mistari mishata katika shairi hili. (alama 2)
e. Eleza muundo wa shairi hili. (alama 4)
f. Huku ukitolea mifano, bainisha uhuru wa kishairi zilizotumiwa na mshairi. (alama 2)
g. Bainisha nafsineni katika shairi hili. (alama 1)
h. Fafanua toni ya shairi hili. (alama 2)

**5. Soma shairi lifuatalo kisha ujibu maswali**

Tusitake kusimama, bila kwanza kutambaa,
Au dede kuwa hima, kabula hatujakaa,
Tutakapo kuchutama, kuinama inafaa,
Tujihimu kujinyima, makubwa kutoyavaa.

Tusitake kuenenda, guu lisipokomaa,
Tujizonge na mikanda, inapochagiza njaa,
Na mazuri tukipenda, ni lazima kuyandaa,
Tujiase kujipinda, kujepusha na balaa.

Tusitake uvulana, au sifa kuzagaa,
Tushikiye nyonga sana, tunuiyapo kupaa,
Kama uwezo hapana, tutolee dagaa,
Tujiase hicho kina, maji yanapojaa.

Tusitake vya wenzetu, walochuma kwa hadaa,
Wanaofyatua vitu, na kisha vikosambaa,
Uwezo hatuna katu, umaskini fazaa,
Tujihimu kula vyetu, siendekeze tamaa.

Mtaka kuiga watu, hufata kubwa rubaa,
Vyao vijaile kwetu, vifaa vingi vifaa,
Tunamezwa na machatu, tusibakishe dhiraa,
Tujihimu kilo chetu, hata kama twapagaa.

(Mohamed, S.A)

Maswali:

a. Eleza ujumbe wa mshairi katika shairi hili. (alama 5)

for free exams visit www.freekcsepastpapers.com

b. Ainisha shairi hili kwa kuzingatia vigezo vifuatavyo: (alama 4)
 (i) Idadi ya vipande katika kila mshororo
 (ii) Idadi ya mishororo katika kila ubeti
 (iii) Mpangilio wa maneno katika kila ubeti
 (iv) Mpangilio wa vina katika beti
c. Andika ubeti wa tano kwa lugha nathari. (alama 4)
d. Andika aina mbili za urudiaji zilizotumiwa katika shairi hili. (alama 2)
e. Bainisha aina tatu za uhuru wa kishairi zilizotumiwa katika shairi hili. (alama 4)
f. Eleza maana ya maneno yafuatayo jinsi yalivyotumiwa: (alama 2)
 (i) Makubwa kutoyavaa
 (ii) Tushikiye nyonga

## SEHEMU D : HADITHI FUPI

***K. Walibora na S.A. Mohamed*** **: Damu Nyeusi na Hadithi Nyingine**

**Shibe Inatumaliza :** *Salma Omar Hamad*

6. " Kwa hakika … wanajituma na kujitutumua kwa uzalendo wa taifa lao."

a. Eleza muktadha wa dondoo hili. (alama 4)
b. Taja na kufafanua sifa zozote nne za warejelewa kwenye dondoo hili. (alama 4)
c. Onyesha kinaya kinachojitokeza kwenye dondoo hili ukirejelea hadithi nzima. (alama 12)

**Mame Bakari:** *Mohammed Khelef Ghassany*

7. "Hapo tena ilimjia ile picha chafu ambayo haijabanduka mpaka leo tokea wakati ule ilipoanza. Aliendelea kuliona lile janadume asilolijua likimvamia na kumbaka ghafla.Kisha likambamiza ardhini na ardhi ikashuhudia ukatili na udhalimu ule. Hadi sasa maskioni mwake anasikia miguno na mingurumo ya lile dubwana la janadume."

a) Fafnua toni inayojitokeza kwenye dondoo hili. (alama 2)

b) Huku ukitoa mifano, bainisha mbinu tatu za kimtindo zinazojitokeza kwenye dondoo. (alama 6)

c) Onyesha athari za ukatili uliotajwa kwenye dondoo. (alama 12)

for free exams visit www.freekcsepastpapers.com

## SEHEMU E : FASIHI SIMULIZI

Kijiji chavuma vishindo,
Vya ngoma na nyimbo.

Kwenye vilima vya kata,
Na mabonde kuliko na mito,
Wamama wanalitafuna,
Watoto na vijana wanaliimba, jina,
Jina la nguli Amali wa Jamali. Jamadali kamili.

Ukoo wake wa mashujaa,
Babuze walisifika sana,
Mikuki na mishale walifua,
Kuihami jamii na riaka,
Na hata magao ya kujisitiri, pindi lijapo pambano.

Leo yeye atamba,
Shujaa wa nguvu za tembo,
Mwamba anayepigana bila silaha yoyote,
Angurumapo mahasimu wanazirai, wanavaa lebasi ya woga hasa,
Wasiwasi unawakumbatia.
Angurumapo simba mcheza nani?
Anapotisha Amali wa Jamali atasimama nani?

Zawadi za kole za nazi,
Na mashuke ya mtama,
Zamiminika kwake kutoka kusini na kaskazini,
Kwa kujuhudi za kuwarejesha mitamba na mafahari,
Kutoka mbali walikotekwa,
Mazizi sasa yana uhai,
Miroromo sasa inasikika tena.

Wengine wanaleta vishazi vya samaki,
Kumtunuku,
Huyu mja mwenye nemsi zisizo na ndweo.

Akida wetu,
Atamvisha taji la ngozi ya duma,
Yenye kipembe cha kifaru,
Atamvisha nguo ya ngozi ya simba.

Maswali:

a. Tambua kipera cha utungo huu na utoe sababu ya jibu lako. (Al 2)
b. Ni sifa gani hukibainisha kipera ulichotaja hapo juu? (Al 5)

for free exams visit www.freekcsepastpapers.com

c. Eleza dhima za kipera hiki katika jamii. (Al 5)
d. Jamii iliyoakisiwa kwenye utungo huu huendeleza shughuli gani za kiuchumi? (Al 4)
e. Fafanua mtindo katika kifungu hiki. (Al 4)

for free exams visit www.freekcsepastpapers.com